

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## SHERIA ZA CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa kinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na kinazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kila mwanachuo anatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo mara baada ya kuripoti chuoni.

---

### 1. TAALUMA

- a. Mwanachuo anatakiwa kuhudhuria chuoni kila siku za masomo na kuwajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa pamoja na kufanya mitihani yote. Kutokuhudhuria darasani au kutofanya mitihani kwa zaidi ya vipindi vitatu bila sababu za msingi ni kosa linaloweza kusababisha kusimamishwa masomo au kufukuzwa chuo.
- b. Mwanachuo anatakiwa kufaulu mitihani kwa kiwango cha daraja "C" (asilimia 60). Kufeli ni kosa na mwanafunzi atachukuliwa hatua za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kuandika barua ya kuahidi kubadilika na kufanya vizuri zaidi.
- c. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani haurusiwi. Atakayebainika atafukuzwa chuo mara moja.
- d. Kutakuwa na Mtihani wa Taifa utakaofanyika mwishoni mwa mwaka. Gharama za mtihani zitatangazwa wakati mtihani unapokaribia.
- e. Ni marufuku kupiga kelele, kusumbua darasani au kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu. Adhabu kali zitatolewa.
- f. Hairuhusiwi kuingia na simu darasani, kutumia simu wakati wa masomo, au kuchaji simu bwenini. Atakayebainika atayang'anywa simu na kupewa adhabu.
- g. Mwanachuo wa bweni haruhusiwi kutoka nje ya eneo la chuo bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi wa darasa. Paredi ya chuo ni lazima saa 11:00 jioni siku za mwisho wa wiki. Kibali cha kutoka nje hakitatolewa baada ya saa 12:00 jioni.
- h. Mwanachuo anatakiwa kutii kengele ya chuo kulingana na ratiba. Kupuuza wito ni utovu wa nidhamu.
- i. Mwanachuo anatakiwa kuheshimu bendera na wimbo wa Taifa.
- j. Kushiriki katika shughuli zote za chuo kama usafi wa mazingira ni wajibu wa kila mwanachuo.
- k. Vipindi vya kujisomea vitafanyika kuanzia saa 2:00 usiku hadi 4:00 usiku. Mahudhurio yatachukuliwa.
- l. Kutakuwa na likizo nne (4) kwa mwaka kulingana na kalenda ya masomo. Hairuhusiwi kubaki chuoni wakati wa likizo bila kibali.
- m. Hairuhusiwi kulala bwenini wakati wa masomo bila kibali cha muuguzi wa chuo au mwalimu wa zamu.

---

## 2. SARE

- a. Mwanachuo anatakiwa kuvaa mavazi ya heshima wakati wote.
- b. Wakati wa michezo, mwanachuo atavaa sare za michezo (tracksuit).
- c. Hairuhusiwi kufuga ndevu, kunyoa mitindo, kuweka dawa nywele, kufuga kucha au kupaka rangi.
- d. Hairuhusiwi kuvaa mapambo masikioni, shingoni, puani au mkononi isipokuwa saa ya mkononi.
- e. Mwanachuo anatakiwa kuwa msafi wakati wote na kuepuka manukato yenye harufu kali.
- f. Wasichana wenye nywele ndefu wazikate zisizidi urefu wa sentimita 0.5 au wasuke mistari ya kawaida.
- g. Wavulana wakate nywele zisizidi sentimita 0.5 na kunyolewa ndevu wakati wote.

---

## 3. NIDHAMU

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanachuo na jamii ni lazima.
- b. Kuheshimu bendera, nembo na wimbo wa Taifa ni wajibu.
- c. Ulevi wa aina yoyote (pombe, sigara, madawa ya kulevya) ni marufuku.
- d. Mahusiano ya kimapenzi chuoni kati ya wanachuo au mtumishi na mwanachuo hayaruhusiwi.
- e. Hairuhusiwi kubeba mimba ukiwa chuoni.
- f. Matusi, ugomvi, kupigana au kufanya fujo ni marufuku.
- g. Wizi na uhalifu haviruhusiwi.
- h. Kugoma au kuchochea mgomo ni marufuku.
- i. Kuharibu mali ya chuo au jamii ni kosa.
- j. Mgeni lazima apate kibali kutoka uongozi wa chuo.
- k. Lugha za mawasiliano ni Kiswahili na Kiingereza tu.

---

## 4. MAZINGIRA

- a. Kila mwanachuo atapanda na kukuza angalau mti mmoja wa kudumu.
- b. Kila mwanachuo atapewa eneo maalum la kulitunza kwa usafi.
- c. Kila mwanachuo atakuwa na zamu ya kufanya usafi katika maeneo mbalimbali ya chuo.
- d. Kila Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi ni muda maalum wa usafi.

---

## 5. MAENEO YASIYORUHUSIWA

- a. Hairuhusiwi kuingia bila ruhusa katika maeneo yafuatayo:
  - i. Ofisi za chuo
  - ii. Bohari
  - iii. Jikoni
  - iv. Baa au klabu zinazouza vileo
  - v. Nyumba za kulala wageni
  - vi. Nyumba za watumishi
  - vii. Bweni la jinsia tofauti
- b. Siku za kutoka nje ya chuo ni Jumamosi kuanzia saa 5:00 asubuhi na Jumapili kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni kwa ruhusa.